


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

Simu: +255 22 211-3139, +255 22  
211 0146-10  
Nukushi: +255 22 2135486  
Tovuti: [www.moe.go.tz](http://www.moe.go.tz)  
Unapojibu Tafadhali Taja:



S.L.P. 9121,  
7 Mtaa wa Magogoni,  
11479 DAR ES SALAAM.

Kumb.Na.ED/OKE/NE/Vol.1/01/73

Tarehe: 19/9/2016

Makatibu Tawala (M)  
Makatibu Tawala (W),  
Wathibiti Wakuu wa Ubora wa Shule (K),  
Wathibiti Wakuu wa Ubora wa Shule (W),  
Wakuu wa Shule zisizo za Serikali,  
**TANZANIA BARA.**

**WARAKA WA ELIMU NA. 4 WA MWAKA 2016  
MWONGOZO WA UUNDAJI WA KAMATI ZA SHULE**

Kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na rekebisho Na. 10 la mwaka 1995 kila shule ya msingi sharti iwe na Kamati ya Shule iliyo hai.

Ufuatiliaji katika shule mbalimbali hapa nchini umebainisha kuwa Kamati nyingi za shule hazipo hai na chache zilizopo hazikidhi matakwa ya utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014. Hivyo basi, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inatoa maelekezo ya uundaji upya wa Kamati za Shule.

**Waraka huu unaelekeza yafuatayo:**

- i. Miongoni mwa wajumbe watakaounda Kamati ya Shule, wawepo wawakilishi wa wajumbe wa Serikali za Vijiji/Mitaa.
- ii. Uteuzi na uchaguzi wa wajumbe wa Kamati za Shule pamoja na sifa nyingine stahiki uzingatie sifa za msingi ambazo ni uwezo wa Kusoma, Kuandika na Kuhesabu.
- iii. Kamati ya shule itachaguliwa na kikao cha wazazi.
- iv. Kamati ya Shule itakuwa na wajumbe kumi na tatu (13) na itafanya kazi kwa muda wa miaka mitatu. Hata hivyo, wajumbe wa Kamati wanaweza kuchaguliwa tena kwa kipindi kingine cha miaka mitatu. Ujumbe katika Kamati utakoma baada ya kipindi cha mihula miwili ya miaka mitatu kwa kila mihula.
- v. **Wajumbe watakaounda Kamati za Shule:**
  - (a) Mwenyekiti: Awe ni mkazi wa eneo hilo na pia awe na cheti cha kuhitimu Elimu ya Sekondari au zaidi.
  - (b) Makamu Mwenyekiti: Awe na sifa kama za Mwenyekiti.
  - (c) Katibu: Atakuwa ni Mwalimu Mkuu wa Shule husika.

